TANGAZO LA SERIKALI NA. 435 la Tarehe 31/5/2024

SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA

(SURA YA 290)

# SHERIA NDOGO

*(Imetengenezwa chini ya Kifungu cha 16(1) )*

MAREKEBISHO YA SHERIA NDOGO YA ADA NA USHURU YA HALMASHAURI YA WILAYA YA MBARALI YA MWAKA, 2024

Jina

T.S Na. 893 la 2023

1. Sheria Ndogo hii itajulikana kama Marekebisho ya Sheria Ndogo ya Ada na Ushuru ya Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali ya mwaka 2024, na itasomwa pamoja na Sheria Ndogo ya Ada na Ushuru ya Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali ya mwaka 2023 ambayo hapa imerejewa kama "Sheria Ndogo Kuu".

Marekebisho ya aya ya 7

2. Sheria Ndogo Kuu inarekebishwa katika aya ya 7 kwa kufuta aya ndogo ya (1) na kuandika upya kama ifuatavyo:

"(1) Kutakuwa na ushuru wa mazao utakaotozwa na Halmashauri kwa mnunuzi wa mazao pindi anunuapo mazao kutoka kwa muuzaji katika eneo la Halmashauri".

Dodoma,
18 Aprili, 2024

MOHAMED OMARY MCHENGERWA
*Waziri wa Nchi- Ofisi ya Rais*
*(Tawala za Mikoa Na Serikali za Mitaa)*